

Nambari ya Mwanafunzi \_\_\_\_\_

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR  
BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR  
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA TATU**

**309**

**STADI YA KUSOMA**

**MUDA: SAA 1:00**

**JUMATATU 06 OKTOBA, 2025 ASUBUHI**

**MAELEKEZO KWA MWANAFUNZI**

- 1. Upimaji huu una sehemu MBILI (2) A na B.**
- 2. Jibu maswali YOTE katika kila sehemu.**
- 3. Andika nambari yako ya upimaji katika kila ukurasa.**
- 4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
- 5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
- 6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha upimaji**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI |       |       |                     |       |       |
|-------------------------------|-------|-------|---------------------|-------|-------|
| NAMBARI<br>YA SWALI           | ALAMA | SAINI | NAMBARI<br>YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. i)                         |       |       | 2.                  |       |       |
| ii)                           |       |       |                     |       |       |
| iii)                          |       |       |                     |       |       |
| iv)                           |       |       |                     |       |       |
| v)                            |       |       |                     |       |       |
| JUMLA                         |       |       | JUMLA               |       |       |
| JUMLA KUU                     |       |       |                     |       |       |
| SAINI YA MHAKIKI              |       |       |                     |       |       |

**Upimaji huu una kurasa 4 zenye maandishi**

**SEHEMU A: (Alama 25)**  
**KUSOMA KWA UFAHAMU**  
**Jibu swali lifuatalo.**

1. Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika herufi ya jawabu sahihi kwenye mabano.

Dawa za kulevya ni dawa zinazoathiri mwili na akili. Serikali inapiga vita matumizi ya dawa za kulevya. Mtu anayetumia dawa hizo hukosa nguvu na kushindwa kufanya kazi. Dawa hizo ni hatari sana. Madhara yake ni mengi. Madhara yake huweza kumpata baba, mama, vijana na watoto. Dawa za kulevya zinaweza kukufanya kuwa mgonjwa. Pia zinaathiri akili ya mtumiaji. Waathirika wakubwa wa dawa za kulevya ni vijana.

Dawa hizo zipo za aina nyingi kama vile bangi, sigara, pombe na heroini. Watoto jiepusheni kutumia dawa hizo ili kulinda afya zenu. Ikiwa mtu atakupa dawa za kulevya kataa na uondoke. Kaa mbali na watu wanaotumia dawa za kulevya. Wanaweza kukushawishi kutumia dawa hizo na kuathiri afya yako. Afya yako ni muhimu sana. Mtoto ni taifa la kesho.

**MASWALI**

- i. Maana ya dawa za kulevya ni ( )
  - A. Dawa za waathirika wa ulevi
  - B. Dawa zinazoathiri mwili
  - C. Dawa zinazotumiwa sana
  
- ii. Kwa sababu gani serikali inapiga vita matumizi ya dawa za kulevya? ( )
  - A. Nguvu kazi itapungua
  - B. Watu watalewa sana
  - C. Zitakufanya kuwa mgonjwa
  
- iii. Madhara makubwa ya dawa za kulevya yanawapata nani? ( )
  - A. Wazazi
  - B. Vijana
  - C. Watoto
  
- iv. Dawa za kulevya zinaathiri ( )
  - A. Afya
  - B. Mtoto
  - C. Wagonjwa
  
- v. Kwanini watoto wanatakiwa kukaa mbali na watumiaji wa dawa za kulevya? ( )
  - A. Wasipate kulewa
  - B. Wasipate kushawishiwa
  - C. Wasipate ugonjwa

**SEHEMU B: (Alama 25)**

**UFUPISHO**

**Jibu swali lifuatalo.**

2. Soma habari ifuatayo kisha fupisha kwa maneno yasiyopungua kumi na nane (**18**) na yasiyozidi ishirini na mbili (**22**).

Siku moja mwalimu wetu wa darasa la tatu aliandaa safari ya kimasomo. Ilikuwa ni mara yetu ya kwanza kwenda safari ya kimasomo. Tulikwenda kutembelea sehemu za kihistoria. Kila mwanafunzi alitakiwa kushiriki ili akajifunze mambo mbalimbali.

Siku ya safari ilipofika kila mwanafunzi alijiandaa vizuri. Tulichukua vyakula pamoja na buku na kalamu kwa ajili ya kuandika atakachojifunza.

Tulipofika sehemu za kihistoria tulikaribishwa vizuri. Tulifahamishwa mambo mengi ya kihistoria. Mwisho tulipelekwa kuangalia wanyama. Baadaye tulikula na kurudi nyumbani tukiwa na furaha.

---

---

---

---

---

---

---

---

=====